* 0000800000001 *

Cambridge Assessment International Education

# Cambridge IGCSE™

CANDIDATE NAME

CENTRE NUMBER | CANDIDATE NUMBER

* 2 0 5 9 9 8 5 4 4 4 *

**SWAHILI** **0262/01**

Paper 1 Reading and Writing **May/June 2025**

**2 hours**

You must answer on the question paper.

No additional materials are needed.

**INSTRUCTIONS**

- Answer **all** questions.
- Use a black or dark blue pen.
- Write your name, centre number and candidate number in the boxes at the top of the page.
- Write your answer to each question in the space provided.
- Do **not** use an erasable pen or correction fluid.
- Do **not** write on any bar codes.
- Dictionaries are **not** allowed.

**INFORMATION**

- The total mark for this paper is 60.
- The number of marks for each question or part question is shown in brackets [ ].

This document has **16** pages. Any blank pages are indicated.


© UCLES 2025

## Zoezi 1

Soma kifungu kifuatacho kutoka kwenye gazeti kinachohusu waanzilishi wa maonyesho ya miundo ya kisanaa na halafu jibu maswali yanayofuata.

Wiki iliyopita nilienda kwenye maonyesho ya miundo ya kisanaa yaliyokuwa katika makumbusho ya kisasa yanayoitwa Louisiana. Nilipoingia tu kwenye ukumbi wa makumbusho, niliona pango lililoundwa kwa mawe meupe. Nilipolisogelea nikagundua kwamba ile taswira ya pango ilijengwa kitaalamu kwa kutumia mawe ya mviringo yaliyokuwa mengi na madogo madogo. Yalikuwa yametundikwa kwa nyuzi nyembamba. Nyuzi hizo hazikuonekana hadi pale mtu alipozikaribia.

Waanzilishi wa maonyesho hayo ni Bwana Kabage Karanja na Bi Stella Mutegi. Mara ya kwanza nilipowaona, Bwana Kabage alikuwa amevaa shuka nyekundu ya kimasai niliyoipenda sana. Watu walikuwa wamemzunguka huku wakiomba kupiga naye picha. Bi Stella alivaa shati la kitenge na suruali nyeusi. Wao wanaishi Nairobi na walisafiri pale kuonyesha kazi yao.

Ingawa waliongelea mambo mengi sana, mimi ninakumbuka mambo mawili zaidi ya yote kwa sababu mambo hayo yanahusu mapango. Kwanza walizungumzia maisha ya binadamu wa kale walioishi kwenye mapango. Enzi hizo, binadamu hawakuwa na miundombinu ambayo tunayo hivi leo. Mimi hufurahia kusoma hadi usiku wa manane kwa sababu taa huwezesha siku ziwe ndefu zaidi. Lakini binadamu hawaelewi kwamba, kuwasha taa kunaathiri maisha ya viumbe wengine ambao wapo duniani.

Hivi sasa watu wanaoishi mijini wanawasha taa majumbani, ofisini na pia barabarani. Jambo la kwanza ambalo tunaliona ni kwamba miili ya binadamu inachoka kwani siku huwa ndefu zaidi ya usiku kutokana na mwanga. Na watu wanaopenda kuona nyota wanashindwa, hasa wanapokuwa mijini.

Jambo la pili ambalo Kabage na Stella waliongelea ni athari za bindamu kwa mazingira. Walikuwa na michoro iliyochorwa na watu wa zamani kwenye kuta za mapango. Sote tuliweza kuona kwamba mazingira yalikuwa tofauti kabisa na ulimwengu wa sasa. Inaonekena kwamba binadamu waliheshimu mazingira yao. Walitoa mfano wa jiji la Nairobi ambapo hadi sasa kuna mbuga ya wanyama katikati ya mji. Hii ni ishara kwamba zamani, binadamu na wanyama hawakuwa na uharibifu kama huu wa hivi sasa.

Katika maonyesho ya miundo ya Kabage na Stella, kuna suluhisho la matatizo haya mawili. Kuhusu taa, wanasema kwamba tusidharau kwamba nishati kubwa inatumika kwa binadamu kupenda kuwasha taa. Wanasema kwamba tujaribu kuchagua aina za taa ambazo haziwadhuru wanyama wadogo na wakubwa. Pia tungeweza kubadili miundo ya taa tunazotumia; jambo litakalopunguza gharama zetu za nishati. Na kuhusu maji, sote tunafahamu umuhimu wa kupanda miti lakini wao wameunda jengo la kutengeneza mvuke kutokana na mbao pamoja na malighafi kutoka kwenye mazingira. Mvuke wa muundo huo hupanda hewani, hugeuka kuwa mawingu na hatimaye mvua hunyesha. Kwa kweli muundo huo umenishangaza sana.



DO NOT WRITE IN THIS MARGIN

DO NOT WRITE IN THIS MARGIN

**1** Mwandishi aliona nini alipowasili kwenye makumbusho?

.......................................................................................................................................... [1]

**2** Kitu gani kilishikilia mawe katika maonyesho?

.......................................................................................................................................... [1]

**3** Mwandishi alivutiwa zaidi na nguo ipi?

.......................................................................................................................................... [1]

**4** Taa ina faida gani ya binafsi kwa mwandishi?

.......................................................................................................................................... [1]

**5** Mwandishi anataja athari zipi za taa kwa binadamu? Taja maelezo **mawili**.

..........................................................................................................................................

.......................................................................................................................................... [2]

**6** Kwa maoni ya Kabage na Stella, kwa nini mazingira ya leo yameharibika?

.......................................................................................................................................... [1]

**7** Kabage na Stella wametengeneza nini kwa sababu ya umuhimu wa mvua?

.......................................................................................................................................... [1]

[Jumla: 8]

## Zoezi 2

Wanafunzi wanne wanazungumza kuhusu ushoni.

### A Ahmed

Ni shangazi yangu aliyenifundisha kushona. Niliishi naye kwa miaka kadhaa na alinifundisha kupika, kushona na hata kufuma. Aliniambia kwamba zamani wao walishona nguo zao wenyewe na kuzivaa. Alifurahi alipoona mimi nilivutiwa na ujuzi huu kwani ni urithi wetu. Bila shaka nilitaka kujifunza kushona lakini nilifurahia zaidi kusikiliza hadithi alizokuwa akinihadithia pale tulipokaa pamoja ili kushona. Nimeweza kuielewa historia ya familia yetu zaidi. Kwa mfano, mitindo ya nguo imebadilika kweli kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Shangazi alipokuwa mtoto alijifunga kanga tu na hakuvaa gauni. Baadaye, alipokuwa kijana, alipenda kushona mitindo ya nguo ambapo mabega yalishonwa kama puto. Mimi ninaona huo mtindo ni kichekesho sasa lakini kwake ulikuwa ni wa kawaida. Sasa nimeamua kuandika blogu mtandaoni inayohusu ushoni na pia kujumuisha masimulizi aliyokuwa akinihadithia. Pia nitatengeneza na kubandika video mbalimbali ili wengine waweze kujifunza kushona na kusikiliza mazungumzo yetu.

### B Belinda

Mara ya kwanza kumwona mtu akishona, ilikuwa kwenye video mtandaoni. Nilipomtazama nilipata motisha kununua vitambaa, uzi, na sindano na nikaanza kushona. Mwanzoni nilifuatilia maelezo hatua kwa hatua kwani nilikuwa na wasiwasi kwamba ningeweza kushona kituko ambacho kingeonekana kama kichekesho. Lakini baada ya muda nikaanza kushona kwa utulivu na pia nikavumbua mbinu zangu mwenyewe za kushona. Tena nikawa natumia aina fulani za vitambaa tu. Kuna vitambaa vingi ambavyo sipendi kutumia kutokana na ugumu wake au urahisi wa kuchanika. Mimi ninatumia vile nivipendavyo tu. Siku hizi nimekuwa mshoni mzuri na ninataka kufanya ushoni kuwa taaluma yangu. Kwa kweli hii si kazi ya mtu mvivu. Nimeamua kujiandikisha kwenye chuo cha sanaa mwaka ujao ili niweze kujiajiri kama mwanamitindo baadaye.

### C Chege

Nimekuwa nikishona kwa muda sasa ingawa haikuwa rahisi kwangu kujifunza ushoni. Nilihisi kwa vile mama yangu ni mshoni maarufu nchini kwetu, na huonekana ametulia kwa furaha anaposhona, basi mimi ningaliweza kujifunza kirahisi sana. Lakini, kutokana na makosa mengi niliyopitia nimegundua kwamba ushoni si ujuzi ambao unazaliwa nao bali inabidi kufanya mazoezi mengi ya mara kwa mara ili kuwa mshoni bora. Pia imenibidi kuenda chuo cha ushoni ili kujifunza zaidi. Baadhi ya vitu ninavyoshona ni nguo za kizamani ambazo watu wengi wameanza kuzipenda siku hizi. Ninafikiri mitindo haipitwi na wakati, kamwe, na watu wavae nguo zilizoshonwa ili mradi ziwape furaha. Nimeanzisha kipindi kinachorushwa mitandaoni ambamo ninaonyesha mitindo tofauti ya kimataifa na umuhimu wa kuvaa unavyotaka. Nimewaalika wanamitindo wengi kwenye kipindi, ingawa ninapenda bidhaa zao, nisingetaka kuwa na ajira yao.

### D Damaris

Kamwe sikutegemea kwamba ningaliweza kujifunza ushoni. Simjui mtu yeyote ambaye anashona. Maisha yangu yote nimekuwa nikipeleka nguo kwa fundi cherehani ili anizibie viraka au anishonee nguo mpya tena hadi sasa ninafanya hivyo ingawa ninaweza kushona vitu rahisi kama foronya na pia mashuka. Sipendi kujichosha na kazi za kushona ingawa nikishona huhisi kama akili yangu inatulia sana na ninapata hisia tofauti kabisa na ile ya wasiwasi ninayokuwa nayo wakati nikifanya kazi zangu za chuo kikuu. Ingawa nina masomo mengi ya chuoni, hata hivyo hupenda kujiburudisha kwa kushona. Tena, kwa vile karibu na nyumba yangu kuna duka kubwa la vitambaa, uzi, na mambo ya kushonea, mimi hupenda kuenda huko na kugusa vitambaa, ingawa sivinunui kwani sina ajira ya kunipa pesa nyingi. Ninahisi kama ushoni ungekuwa na masharti machache ningalishona zaidi.



DO NOT WRITE IN THIS MARGIN

DO NOT WRITE IN THIS MARGIN



Soma taarifa (**8–16**) zifuatazo. Weka alama ya tiki (✓) kwenye kisanduku kuonyesha aya (**A–D**) inayohusiana na kila taarifa. Kuna mfano mmoja hapa chini.

**Mfano**

Mwanafunzi yupi…

alifundishwa ushoni na familia yake?

**A** ☑ **B** ☐ **C** ☐ **D** ☐

**8** anahisi mitindo ya zamani inachekesha?

**A** ☐ **B** ☐ **C** ☐ **D** ☐ [1]

**9** ana masharti mengi kuhusu ushoni?

**A** ☐ **B** ☐ **C** ☐ **D** ☐ [1]

**10** aligundua huwezi kurithi ujuzi wa kushona?

**A** ☐ **B** ☐ **C** ☐ **D** ☐ [1]

**11** amefanya mafunzo ya ushoni katika taasisi ya elimu?

**A** ☐ **B** ☐ **C** ☐ **D** ☐ [1]

**12** anahisi utulivu anaposhika vifaa vya kushona?

**A** ☐ **B** ☐ **C** ☐ **D** ☐ [1]

**13** ana uvivu wa kushona?

**A** ☐ **B** ☐ **C** ☐ **D** ☐ [1]

**14** anapanua ufahamu wake wa historia?

**A** ☐ **B** ☐ **C** ☐ **D** ☐ [1]

© UCLES 2025

**15** alipata motisha ya kushona mtandaoni?

**A** ☐ **B** ☐ **C** ☐ **D** ☐ [1]

**16** atategemea ushoni ili kukidhi mahitaji ya maisha?

**A** ☐ **B** ☐ **C** ☐ **D** ☐ [1]

[Jumla: 9]

DO NOT WRITE IN THIS MARGIN

DO NOT WRITE IN THIS MARGIN
DO NOT WRITE IN THIS MARGIN
DO NOT WRITE IN THIS MARGIN
DO NOT WRITE IN THIS MARGIN
DO NOT WRITE IN THIS MARGIN

**PLEASE TURN OVER FOR EXERCISE 3**

© UCLES 2025

## Zoezi 3

Soma makala yafuatayo kuhusu nyumba nduchu.

Ulimwenguni pote, watu wanaishi katika nyumba za kila namna.

Content removed due to copyright restrictions.

Ninahisi kwamba kwa watu wazima jambo hili litachosha sana kwani huwafanya wawe wapweke na wakose ujirani mwema.



DO NOT WRITE IN THIS MARGIN
DO NOT WRITE IN THIS MARGIN
DO NOT WRITE IN THIS MARGIN
DO NOT WRITE IN THIS MARGIN
DO NOT WRITE IN THIS MARGIN

DO NOT WRITE IN THIS MARGIN



Andika maelezo mafupi chini ya vichwa vya habari (**17–19**) vinavyotokana na makala uliyoyasoma.

**17** Hisia za mwandishi kuhusu yeye kuishi kwenye nyumba nduchu:

- ..........................................................................................................................
- ..........................................................................................................................
- ..........................................................................................................................

[3]

**18** Mawazo ya watu wazima kuhusu kuishi kwenye nyumba nduchu:

- ..........................................................................................................................
- ..........................................................................................................................
- ..........................................................................................................................

[3]

**19** Ushahidi wa umuhimu wa mazingira kwa nyumba nduchu:

- ..........................................................................................................................
- ..........................................................................................................................
- ..........................................................................................................................

[3]

[Jumla: 9]

Katika zoezi 4, utatumia maelezo haya kutunga ufupisho.

## Zoezi 4

**20** Sasa tunga ufupisho wa faida na hasara za nyumba nduchu. Unaweza kutumia maelezo yako mengine kutoka zoezi 3 ili kukusaidia.

Ufupisho wako usizidi **maneno 100**.

Tumia maneno yako mwenyewe kadiri iwezekanavyo.

Utapata alama zisizozidi 4 kwa maudhui ya ufupisho wako, na alama zisizozidi 6 kwa lugha makini na sahihi.

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

[Jumla: 10]

DO NOT WRITE IN THIS MARGIN

DO NOT WRITE IN THIS MARGIN



## Zoezi 5

**21** Umepata nafasi ya kutoa maelezo kuhusu uwanja wa michezo uliopo katika mji unaoishi. Andika blogu itakayosomwa na watu duniani pote. Unapaswa kutaja:

- Aina ya uwanja mjini kwako
- Mawazo yako kuhusu uwanja wa michezo
- Shughuli zinazofanywa kwenye uwanja wa michezo

Blogu yako isizidi **maneno 120**.

Utapata alama zisizozidi 3 kwa maudhui ya blogu yako, na alama zisizozidi 5 kwa mtindo na umakini wa matumizi ya lugha yako.

[Jumla: 8]

## Zoezi 6

**22 ‘Tamasha la filamu la taifa lisionyeshe filamu kutoka nje ya nchi.’**

Je, unakubaliana na wazo hili?

Andika makala katika gazeti la shule ili kutoa maoni yako. Makala yasizidi **maneno 200**.

Kuna fahari ya kuonyesha waigizaji kutoka nchini kwako tu.

Katika dunia ya utandawazi ni muhimu kuwa na matamasha ya kimataifa!

Unaweza kutumia maoni ya hapo juu, na pia ni lazima kutumia mawazo yako mwenyewe.

Utapata alama zisizozidi 8 kwa maudhui ya makala, na alama zisizozidi 8 kwa mtindo na umakini wa matumizi ya lugha yako.



DO NOT WRITE IN THIS MARGIN

[Jumla: 16]

DO NOT WRITE IN THIS MARGIN

BLANK PAGE

DO NOT WRITE IN THIS MARGIN

BLANK PAGE

DO NOT WRITE IN THIS MARGIN

© UCLES 2025

BLANK PAGE

DO NOT WRITE IN THIS MARGIN DO NOT WRITE IN THIS MARGIN DO NOT WRITE IN THIS MARGIN DO NOT WRITE IN THIS MARGIN DO NOT WRITE IN THIS MARGIN

Permission to reproduce items where third-party owned material protected by copyright is included has been sought and cleared where possible. Every reasonable effort has been made by the publisher (UCLES) to trace copyright holders, but if any items requiring clearance have unwittingly been included, the publisher will be pleased to make amends at the earliest possible opportunity.

To avoid the issue of disclosure of answer-related information to candidates, all copyright acknowledgements are reproduced online in the Cambridge Assessment International Education Copyright Acknowledgements Booklet. This is produced for each series of examinations and is freely available to download at www.cambridgeinternational.org after the live examination series.

Cambridge Assessment International Education is part of Cambridge Assessment. Cambridge Assessment is the brand name of the University of Cambridge Local Examinations Syndicate (UCLES), which is a department of the University of Cambridge.